
# SHARKS & RAYS


## PAPA NA TAA





Papa na Taa wa Afrika mashariki, makazi yao, umuhimu na Hatari zinazowakumba.





# Wahisani

**CORDIO East Africa:** Peter Musembi, Dkt. Melita Samoilys

**Coral Reef Care:** Rolf Voorhuis

**Mbunifu wa picha, Kielelezo na mpango**: Frank Rogan, Bado Blak



Mwongozo wa utangulizi wa Papa na Taa wa Mwambao wa Afrika mashariki wanaoonekana kwa urahisi, umeundwa kuhamasisha hitahi la kuhifadhi na kulinda papa na taa wa afrika mashariki.


Mwongozo huu pia hutumika kuonyesha aina mbalimbali za papa na taa wanaopatikana katika mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki, makazi yao na vitishio. Hitaji letu ni kuondoa dhana potofu,kueleza ukweli na kuhamasisha watu katika mwambao wa pwani ili kuchangia kwa kueleweka kwa aina za papa na taa.

Hiki kitabu kinaweza kusambazwa bila malipo kwa shule, jamii za pwani na wahusika wote wenye nia.

2021

CORDIO

CORAL REEF CARE



# Yaliyomo

**Utangulizi**........................................4
Umuhimu wa papa na taa........................................4

**Makazi ya papa na taa**........................................5
**Kufisha imani potofu kuhusu papa**........................................6
Makundi ya vitisho kwa papa na taa........................................6

**Aina ya kawaida ya papa na taa wa Afrika Mashariki**........................................7
Pezu mweusi........................................7
Papa Mbingusi,Papa Shilingi,Tezi Madebe........................................8
Papa Kijivu,Papa Sumbwe,Marimbe........................................9
Papa Shiruanzi,Papa Chindi,Papa Charawanza........................................10
Nyenga, Taa chui, Kipungu........................................11

**Tishio kwa papa na taa**........................................12
**Marejeleo**........................................13



## UTANGULIZI

Papa na taa wana mchango mkubwa katika kuhifadhi mfumo ikolojia wa baharini na pwani. Wanapatikana katika bahari za ulimwenhu mzima na katika makazi mbalimbali kama vile bahari wazi, miamba ya matumbawe, nyasi za baharini, misitu ya mikoko na mito.

Pamoja na umuhimu wao, papa hudhaniwa kuwa viumbe wa ajabu na wa kuogofya baharini. Mwongozo huu unanuia kuondoa dhana potofu huku ikieleza ukweli ili kusaidia watu kuelewa tabia jumla za papa na hitaji la kuhifadhi samaki hawa muhimu.




## UMUHIMU WA PAPA NA TAA

Papa na taa ni muhimu kwa mazingira na jamii kupitia njia zifuatazo:

- Kama wawindaji wakubwa, huweka mazingira safi kwa kula wanyama wagonjwa na dhaifu na kudumisha usawa wa wanyama wanaowinda wanyama wengine katika viwango vya chini. Kutokuwa na papa na taa baharini ni kama savanna bila simba, mfumo wa ikolojia utakuwa nje ya udhibiti
- Aina zote za papa na taa ni kivutio katika sekta ya utalii ya kupiga mbizi. Kwa mfano, aina kama vile papa shilingi, kipungu na taa mobula hupendwa na wapiga mbizi wengi.


Papa na taa wamekuwepo kwa hadi miaka milioni 400 na hii inawafanya kuwa mmoja ya aina ya viumbe wazee wanaoishi kwenye sayari. Hata hivyo, kwa sababu ya viwango vya chini vya uzazi na kuongezeka kwa vitisho kama vile kuvuliwa kupindukia, idadi yao imeendelea kupungua kwa muda.





## Makazi ya papa na taa

Papa na taa hukaa katika makazi yafuatayo: miamba ya matumbawe,maeneo ya mawimbi ya misitu ya mikoko, nyasi za baharini,mito na bahari wazi




## miamba ya matumbawe

Miamba ya matumbawe imesambazwa sana katika pwani ya Afrika Mashariki isipokuwa pale ambapo miisho mikubwa ya mito huingia baharin mahali ambapo miamba huvunjika. Papa na taa kama vile pezu mweusi, papa shiruanzi, papa wa kijivu, nyenga wanaweza kupatikana katika miamba ya matumbawe


## Misitu ya mikoko

Mikoko hupatikana kando ya eneo la katikati ya mawimbi katika maeneo kadhaa kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Baadhi ya aina za papa na taa kama vile papa sumbwe, pezu mweusi na baadhi ya taa hutumia makazi ya mikoko kama kitalu na viwanja vya kulisha.









## Nyasi za baharini

Nyasi za baharini ni makazi ya kawaida katika mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki na baadhi ya papa na taa hutumia nyasi za bahari kama makazi ya lishe.





## Mito


Milango ya mito ni makazi ambayo hutengenezwa wakati ambapo mito huungana na bahari. Papa na taa ikiwa ni pamoja na samaki wa mbao ambao ni nadra kuwapata hukaa katika makazi haya. Papa charawanza adimu anaweza






## Bahari wazi

Papa wa Pelagic kama vile Papa mbingusi, Papa shiruanzi na Mako papa hupatikana katika bahari wazi





## Kufisha imani Potofu kuhusu Papa na Taa

Kinyume na imani maarufu, papa si wanyama wala watu kama inavyoonyeshwa katika sinema mbalimbali au inavyosimuliwa katika hadithi nyingi. Kwa kweli, Aina nyingi ya Papa hawana madhara iwapo hawajachokozwa.

Aina nyingi ya Papa na Taa huona haya na si hatari kwa wanadamu. Hatahivyo,mtu anapaswa kufahamu uwezo wa kila wakati wa tabia ya wanyama kujikinga kutokana na sababu kama vile uwepo wa chakula,kujamiana na kulinda eneo lao.

Papa ni walaji nyama na hula samaki, krestasia (samaki kama vile kaa na kamba), moluska (pweza na ngisi) na wanyama wengine wasio na uti wa mgongo. Baadhi ya papa wakubwa kama vile papa Shilingi, na taa kama vile kipungu ni vichujio wanaolisha viumbe wanaoelea juu ya uso wa bahari.

## Hali ya tishio la papa na taa


Aina nyingi ya papa na taa wamo hatarini. Kategoria mbalimbali za hali ya tishio kuanzia kutoweka (EX) mpaka  wasiwasi mdogo(LC) ni taarifa na tathmini ya tafiti za spishi. Aina 13 zinazopatikana kwa urahisi katika mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki wameathirika kwa njia tofauti huku wengi wa papa na Taa hawa wakiwa hatarini.


Baadhi ya shughuli zinazotishia ukuwaji wa Papa na Taa ni pamoja na,Uvuvi haribifu,kukata Pezi za papa,uharibifu wa makazi na uchafuzi wa mazingira. Hasa, papa mbingusi  na papa charawanza waliohatarini kutoweka huvuliwa kwa ajili ya nyama na mapezi yao.

Papa Shilingi aliyehatarini kutoweka huvuliwa kwa mafuta yake ya ini ambayo mara nyingi hutumiwa katika ujenzi wa mashua za kitamaduni. Katika baadhi ya matukio, samaki hawa wakubwa lakini wapole wamenaswa ili kuruhusu wapiga mbizi kuogelea karibu nao.

Papa na Taa wengine wa kawaida huvuliwa sanasana kwa nyama au kwa bahati nasinu kwenye nyavu kubwa.Mabadiliko ya Tabia nchi pia huathiri Papa na Taa hawa huku maji ya bahari yakibadilika kuwa tindikali au makazi yanaharibiwa kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa au maendeleo ya pwani.

Tunaweza kuhitimisha kwa kusema,Papa na Taa wengi wamohatarini inayosababishwa na shughuli za kibinadamu. Hivyo basi,ni wajibu wetu kuhamasisha juu ya hitaji la kulinda Aina mbalimbali za Papa na Taa






## Aina ya kwaida ya papa na taa wa Afrika Mashariki

Kuna takriban papa 120 na aina 69 za taa waliorekodiwa katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, ni wachache tu kati ya hawa wanaoonekana kwa urahisi na wapiga mbizi au kuvuliwa na wavuvi. Katika mwongozo huu, aina 13 za kawaida zimeonyeshwa ikijumuisha maelezo kama vile jina la Asili na la kisayansi, urefu wa juu zaidi ambao papa anaweza kukua na makazi na tabia zao zinazohusiana.

**kategoria za vitisho vya spishi za IUCN**




VU
Hatarini



### Pezu mweusi


Jina la Asili: Pezi Mweusi | jina la kisayansi: Carcharhinus melanopterus

**Urefu wa juu:** 180cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na miamba

Pezu weusi hula samaki wadogo, sefalopodi (pweza na ngisi) na crustaceans (kaa na samaki-gamba wengine). Spishi hizi ni muhimu katika sekta ya upigaji mbizi.

**CR**

Waliohatarini sana



## Papa mbingusi

Jina la Asili: Papa Mbingusi
jina la kisayansi: Sphyrna lewini

**Urefu wa juu:** 400cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na bahari wazi


Papa mbingusi hula samaki na sefalopodi (pweza na ngisi)

**EN**

Waliohatarini

## Papa shilingi

Jina la Asili: Papa Shilingi
Jina la kisayansi: Rhincodon typus




**Urefu wa juu:** 1200cm
**Makazi yanayohusiana:**
bahari ya wazi na miamba ya matumbawe ya pwani

Papa shilingi hula planktoni, krestasia wa planktoni na samaki wadogo. Papa shilingi ni maarufu kwa shughuli za utalii mazingira kama vile kuogelea kwa kupiga mbizi.

**NT**

Karibu kutishiwa



## Pezi madebe


Jina la Asili: Pezi Madebe
Jina la kisayansi: Galeocerdo cuvier

**Urefu wa juu:** 600cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na bahari ya wazi

Pezi madebe hula samaki, sefalopodi(pweza na ngisi) kasa wa baharini, mamalia wa baharini na ndege wa baharini.

EN

Waliohatarini



## Papa kijivu

Jina la Asili: Papa Kijivu
Jina la kisayansi: Carcharhinus amblyrhynchos

**Urefu wa juu:** 250cm
**Makazi yanayohusiana:**
pwani na miamba ya matumbawe

Papa wa kijivu ni mojawapo ya papa wanaopatikana kwa urahisi kwenye miamba. Sana Sana,wao hula samaki, pweza, ngisi na crustaceans kama vile kamba na kaa. Wao ni wadadisi na wameju-

VU

Hatarini



## Papa sumbwe

Jina la Asili: Papa Sumbwe
Jina la kisayansi: Carcharhinus

**Urefu wa juu:** 340cm
**Makazi yanayohusiana:**
pwani na mtoni

Lishe ya papa sumbwe hujuisha samaki wenye mifupa, papa wengine (elasmobrachs) pweza na ngisi (sefalopodi) na mamalia wa baharini. Pia wanajulikana kulinda maeneo yao.

VU

Hatarini

## Marimbe

Jina la Asili: Marimbe
Jina la kisayansi: Carcharhinus albimaginatus

**Urefu wa juu:** 300cm
**Makazi yanayohusiana:**
pwani na miamba

Marimbe hula samaki wenye mifupa, papa wadogo, pweza na ngisi




VU

Hatarini

## Papa siruanzi

Jina la Asili: Papa Siruanzi
Jina la kisayansi: Triaenodon obesus



**Urefu wa juu:** 160cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na miamba ya matumbawe

Papa shiruanzi hula samaki wadogo, pweza na ngisi(cephalopods) na krasteshia kama vile kaa na kamba. Spishi hizi ni wadadisi sana na zimejulikana kuwakaribia wapiga mbizi na wavuvi wa kupiga mbizi kwa mikuki.

EN


Waliohatarini

## Papa chindi

Jina la Asili: Papa Chindi
Jina la kisayansi: Stegostoma tigrinum

**Urefu wa juu:** 235cm
**Makazi yanayohusiana:** chini ya mchanga na miteremko ya miamba ya nje

papa chindi hula krasteshia wa moluska na samaki wenye mifupawa kupiga mbizi kwa mikuki.



CR

Waliohatarini sana



## Papa charawanza

Jina la Asili: Papa Charawanza
Jina la kisayansi: Rhynchobatus djiddensis

**Urefu wa juu:** 300cm
**Makazi yanayohusiana:** maeneo ya pwani na mchanga yenye kina kifupi

Papa charawanza hula samaki wenye mifupa, moluska na krasteshia (kaa, kamba)

LC


Wasiwasi mdogo

## Nyenga

Jina la Asili :Nyenga
Jina la kisayansi: Taeniura hymma


**Urefu wa juu:** 70cm
**Makazi yanayohusiana:**
maeneo ya mchanga yenye kina kifupi na sehemu za nyasi za baharini

Kipungu hula bivalves, sefalopodi, krasteshia na samaki wadogo wa mifupa. Wana uti wa mgongo wenye sumu karibu na msingi wa mkia ambao unaweza kusababisha majeraha.



EN

Waliohatarini



## Kipungu

Jina la Asili: Kipungu/Taachui
Jina la kisayansi: Aetobotus narinari

**Urefu wa juu:** 330cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na miamba

Kipungu hula bivalves, sefalopodi, krasteshia na samaki wadogo wa mifupa. Wana uti wa mgongo wenye sumu karibu na msingi wa mkia ambao unaweza kusa-

VU


Hatarini

## Taachui

Jina la Asili: Taachui
Jina la kisayansi: Manta alfredi


**Urefu wa juu:** 500cm
**Makazi yanayohusiana:** pwani na karibu na miamba ya matumbawe

Taachui hula pelagiki(bahari ya wazi) zooplanktoni na samaki wadogo wa pelagiki. Wao ni muhimu kwa sekta ya kupiga mbizi.




# TISHIO KWA PAPA NA TAA

Vitisho vikubwa kwa papa na taa ni pamoja na uvuvi wa kupita kiasi, Uvuvi nasibu,uvuvi wa zana haribifu za uvuvi, uvuvi wa kukata pezi za papa, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa makazi na mabadiliko ya hali ya tabia nchi.



## Zana Haribifu Za uvuvi


Papa na taa hunaswa kwa urahisi katika nyavu za kuvulia samaki zenye matundu madogo na makubwa






## Uvuvi Wa Kupitiliza

Papa na taa hutumiwa kwa nyama, ngozi na wengine hukamatwa wakiwa hai kwaajili ya ufugaji katika matangisamaki. Hii husababisha kupungua kwa idadi ya papa na taa.



## Uchafu wa mazingira

Uchafuzi kutoka kwa taka ngumu, utupaji wa maji taka, plastiki na kemikali ni hatari kwa papa na taa.



## Ukataji Wa Pezi Za Papa

Hii ni shughuli ya kikatili ya kuwinda papa kwa mapezi yao. Mapezi hukatwa na papa hutupwa baharini wakiwa hai ambapo huvuja damu au kuzama na kufa.


## Uharibifu wa makazi


Maendeleo ya pwani na mabadiliko ya tabia nchi yanasababisha uharibifu mkubwa wa makazi ya papa na taa, haswa matumbawe na misitu ya mikoko.




## Marejeleo

Jeremy Kiszka, Jean-Pascal Qoud & Per Berggren. 2016. Sharks and Rays: A Field Guide to the Common Elasmobranchs of East Africa. WIOMSA. Zanzibar, Tanzania.







CORDIO East Africa | Coral Reef Care
Design and Illustrations: Bado Blak
2021